# TANGAZO

SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWA KUSHIRIKIANA NA SERIKALI YA JAMHURI YA MALAWI ZINAANDAA KONGAMANO LA BIASHARA NA UWEKEZAJI KATI YA TANZANIA NA MALAWI LITAKALOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA TUGHIMBE ULIOPO MWANJELWA JIJINI MBEYA KUANZIA ***TAREHE 26 HADI 27 JULAI, 2018.***

KONGAMANO HILI LINARATIBIWA NA MAMLAKA YA MAENDELEO YA BIASHARA TANZANIA (TanTrade) NA OFISI YA MKUU WA MKOA WA MBEYA PAMOJA NA KITUO CHA UWEKEZAJI NA BIASHARA KUTOKA MALAWI. KAULI MBIU YA KONGAMANO HILI NI "***KUIMARISHA UHUSIANO WA BIASHARA NA UWEKEZAJI*** ".

LENGO LA KONGAMANO NI KUWAUNGANISHA WAFANYABIASHARA WA TANZANIA NA MALAWI KUTUMIA FURSA ZA BIASHARA NA UWEKEZAJI PAMOJA NA KUKUZA MAHUSIANO BAINA YA NCHI HIZI MBILI.

HAKUNA GHARAMA ZA USHIRIKI. WAHI KUJIANDIKISHA KWA KUPAKUA FOMU KUPITIA TOVUTI YA www.tantrade.or.tz. MWISHO WA KURUDISHA FOMU NI TAREHE 29 JUNI, 2018.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI:**

TAFADHALI PIGA SIMU KUPITIA NAMBA 0713-274653 NA 0767-396924. BARUA PEPE info@tantrade.go.tz. PIA UNAWEZA KUTEMBELEA OFISI ZA TANTRADE ZILIZOPO UWANJA WA MAONESHO YA BIASHARA WA MWL. JULIUS K. NYERERE, BARABARA YA KILWA, TEMEKE - DAR ES SALAAM AU OFISI YA MKUU WA MKOA WA MBEYA ILIYOPO MTAA WA UZUNGUNI, MBEYA.

WOTE MNAKARIBISHWA

